SEHEMU YA 4
JINSI YA KUWAOMBEA WAPOTEVU

LENGO: KUMWOMBA MUNGU AHUSIKE KATIKA JUHUDI ZETU ZA KUENEZA INJILI KABLA NA TUNAPOTEKELEZA WAJIBU HUO (Waroma 10:1)

1. KWA NINI JUHUDI ZA KIINJILI MARA NYINGI HAZIOKOI ROHO NYINGI?

A. Wakristo wengi wanashuhudia wakienda kama wamishenari, wakihubiri na kwa uaminifu wakiwaalika wasioamini wamkubali Yesu, lakini wanafadhaishwa kwa sababu hakuna matokeo. Kwa nini?

B. Jibu ni kwamba wameshindwa kumshirikisha Mungu kikamilifu, kupitia sala, katika juhudi zao za kuokoa Roho.
   1. Sala humleta mwenyezi Mungu katika jitihada za kuokoa roho kutoka utawala wa shetani na kuzihamishia katika ufalme wa Mungu.

   2. Mungu hutenda katika mioyo yetu kulingana na vile tunavyoomba.

II MBONA TWAHITAJI KUOMBA KABLA YA KUANZA KUENEZA INJILI?

A. Kabla ya kuanza kushiriki katika Yesu pamoja na asiyeamini twahitaji kuomba sana.
   1. Mbegu, wakati, nguvu, na hazina muhimu za kiinjili hupotezwa kwa sababu hatusali kikamilifu, tukimwomba Mungu atutangulie, na kuitayarisha mioyo.
   2. Lazima tutangulie upanzi wa mbegu ya injili kwa sala kabla ya uenezi wa injili.
   3. Hii ni muhimu ikiwa tutashiriki katika Yesu kibinafsi kwa kutoa ushuhuda, kuhubiri, matangazo ya radio au runinga (televisheni), au njia nyingine zo zote za kuwafikia wapotevu.

B. Kwa kuwa kueneza injili ni kuzikomboa roho zilizopotea kutoka utawala wa shetani, zipo sala maalum za kivita tunazohitaji kusali.

   a. Katika mfano wake juu ya aina nne za udongo, Yesu alifundisha kwamba wakati mbegu iliyotapanywa (neno) yaanguka njiani, ndege mara moja huila.
   b. Ufunuzi wa Yesu kuhusu mfano huu kwa wafuasi wake:
   "Mbegu ni neno la Mungu. Zile zilizoanguka njiani zaonyesha watu wale wanaosikia lile neno; kisha shetani akaja na kuliondoa mioyoni mwao, wasije wakaamini, na hivyo wakaokoka. Luka 8:11-12

   c. Kwa hivyo kabla hatujatapanya mbegu yetu ya injili, twahitaji kumwomba Mungu aitangulie mbegu yetu ili kuunyosha na kutayarisha moyo wa yule atakayesikia, ili mbegu iote na shetani hataweza kuinyakua kabla haijaokolewa.

2. Shetani hupofusha mawazo ya wasioamini.
   a. Ujanja mwingine wa shetani ambao kwao tungesali kabla ya kueneza injili ni kufunika mawazo ya wale ambao hawajaokoka ili wasiweze hata kuuona mwanga wa injili.
   "Maana, kama injili tunayoihubiri imefichika, imefichika kwa wale wanaopotea. Hata hawaamini kwa sababu yule Mungu wa ulimwengu huu amezitia giza akili zao wasipate kuuona wazi mwanga wa habari njema ya utukufu wa Kristo." 2 Wakorinto 4:3-4.

III KWA NINI SALA NI MUHIMU UNAPOLIHUBIRI NENO LA MUNGU?

A. Hatupasi kuzitegemea njia ambazo tumejifunza kwa moyo, au mahubiri yenye akili, bali tu nguvu za Mungu kwa kuwa ndiye pekee awezaye kuokoa.

B. Mashindano makali yasiyo ya kawaida huenda yakaendelea wakati twampeleka mtu kwake Yesu, kwa hivyo twapasa kumtegemea Mungu wala sio sisi wenyewe.
   1. Iwapo yapo mashindano ya kumkubali Yesu wakati mtu yuwajaribu kufanya hivyo, mwombe mungu auondoe upovu wa shetani na uwezo wo wote shetani aweza kuwa nao juu yao.
   2. Kisha dai damu ya Yesu katika jina la Yesu dhidi ya shetani. Mwambie shetani yuwajua Yesu ndiye mshindi, na yuwajua hawezi kustahimili uwezo wa jina na damu ya Yesu.
   3. Ukijua kwamba unaomba mapenzi yake Mungu ili waokoke (2 Petero 3:9), mwombe Mungu awaokoe.

IV. MUNGU AMETUPATIA SILAHA ZIPI KATIKA VITA HIVI?

A. Kwa kuwa vita hivi vya kuokoa mioyo ni vya kiroho, silaha za akili na nguvu za kibinadamu, kamwe haziwezi kuleta ushindi.

B. Twahitaji silaha zisizo za kidunia katika mapambano haya ya kiroho.

"Kweli tunaishi duniani, lakini hatupigani vita kidunia, maana silaha tunazotumia katika vita vyetu si silaha za kidunia, ila ni nguvu za Mungu zenye kuharibu ngome zote. Tunaharibu hata hoja zote za uwongo." 2 Wakorinto 10:3-4.

C. Mungu ametupatia silaha zipi?
   1. Sala. Yakobo 5:16
   2. Neno la Mungu, upanga wa kiroho. Waefeso 16:17.
      a. Msingi wa sala zote za kueneza injili uwe neno la Mungu.
      b. Tumia injili kumpinga shetani, jinsi Yesu alivyofanya katika majaribio yake. (Matayo 4:4,7,10)

V. MAMLAKA YETU KATIKA MAOMBI YA KUENEZA INJILI NI YAPI?

A. Yesu alitoa viwango vipya viwili vya mamlaka alipokuja duniani, akafa na kufufuka.
   1. Jina la Yesu.
      "Mpaka sasa hamjaomba cho chote kwa jina langu. Ombeni, nanyi mtapata ili furaha yenu ikamilike." Yohana 16:24.

      a. Jina la Yesu ni muhimu kwa sababu yeye mwenyewe, pamoja na mamlaka yake ni muhimu.

      "Kwa sababu hiyo, Mungu alimkweza juu kabisa, akampa jina lililo kuu zaidi kuliko majina yote, ili kwa heshima ya jina la Yesu, viumbe vyote mbinguni, duniani na kuzimu, vipige magoti mbele yake; na kila mtu akiri kwamba Yesu Kristo ni Bwana kwa utukufu wa Mungu Baba." Wafilipi 2:9-11.

b. Watu waweza kuokoka tu katika jina la Yesu, si katika mashirika, kanisa au madhehebu.

"Wokovu haupatikani kwa mtu mwingine ye yote, kwa maana duniani pote, binadamu hawakupewa jina la mtu mwingine ambaye sisi tunaweza kuokolewa naye." Matendo 4:12.

"Atajifungua mtoto wa kiume nawe utampa jina la Yesu, maana yeye atawaokoa watu wake kutoka dhambi zao." Matayo 1:21.

2. Damu ya Yesu.
   a. Ni damu ya Yesu iliyotoa wokovu kwa wale ambao tunawahubiria waje kwa Yesu. *"Maana kwa damu yake Kristo, sisi tunakombolewa."* Waefeso 1:7 (Soma Ufunuo 1:5, Waroma 5:9)

   "Maana mnajua kwamba ninyi mlikombolewa katika mwenendo wenu usiofaa ambao mliupokea kutoka kwa wazee wenu, si kwa vitu vya kuharibika; kwa fedha na dhahabu."

   b. Wimbo mpya waliomwimbia Yesu, mwana kondoo ulihusu watu tunaojaribu kuwafikishia neno la Mungu, waliponunuliwa kwa damu ya Yesu.

   "Wewe unastahili kukitwaa hicho kitabu na kuivunja mihuri yake. Kwa sababu wewe umechinjwa, na kwa damu yako umemnunulia Mungu watu kutoka kila kabila, lugha, jamaa, na taifa. Ufunuo 5:9

   c. Ni mamlaka yetu juu ya shetani.

   "Basi joka hili kuu likatupwa nje. (Joka hilo ndiye yule nyoka wa kale ambaye huitwa pia ibilisi au shetani) kwa sababu ya damu ya mwana kondoo. Ufunuo 12:9,11.

B. Katika utenzi wake mkubwa katika Matayo 28: 18-20, Yesu alisema anatutuma ulimwenguni kote kwa sababu alipewa mamlaka yote.

VI. TWAWEZA KUTUMIA NJIA ZIPI KWA MAOMBI YA KUENEZA INJILI?

A. KWA WALIOKO KARIBU NAWE.

1. **SALA YA VIKUNDI VYA WATU WATATU NDIYO NJIA YA MAOBI YENYE NGUVU ZAIDI KABLA YA UENEZI WA INJILI, AMBAYO TWAWAHIMIZA WATU WOTE WA USHIRIKA WA MWAKA 2000 KUTUMIA.**
   a. Ungana na Wakristo wengine wawili, kila mmoja wenu akichagua watu watatu wasiokuwa Wakristo ambao nyote mtawaombea ili wampate Yesu kuwa mwokozi na Bwana. (Jumla ya wasiookoka - 9)
   b. Muwe mkikutana kila juma kwa dakika 15 kuwaombea watu wenu 9 ili wapate kuokoka.
   c. Tazama maswali na majibu kwa vikundi vya watu watatu kwa masharti kamili kwa maombi ya vikundi vya watu watatu, ukurasa 22.
2. Makundi ya sala mbali na mikutano ya sala ya kikundi chako cha watatu, pamoja na ya kanisa na shirika, ni njia zinazofaa kuwaombea wapotevu.
3. Kusali kwa uaminifu katika wakati wako binafsi wa maombi kila siku ni njia inayoleta matokeo.
4. Tumia njia nyingine yo yote inayofaa kuwaombea wapotevu walioko karibu nawe.

5. HAKIKISHA KWAMBA UNAFUNGA KULA UNAPOWAOMBEA WAPOTEVU HUKU MUNGU AKIONGOZA.

B. KWA WALE AMBAO KAMWE HAWAJASIKIA KUHUSU YESU KOTE ULIMWENGUNI.
   1. Sali, ukimwomba Mungu auelekeze moyo wako kwa taifa ambapo jina la Yesu kamwe halijasikika au ni haba.
      a. Waweza kuwasiliana na viongozi wa ushirika wa mwaka 2000 au mwakilishi wa ushirika wa wanawake kwa ushauri.
      b. Soma 'dirisha 10-40 katika kitabu hiki kujua walipo watu ambao hawajafikiwa na neno la Mungu; lakini kubali taifa, kabila au mji wowote unaopewa na Mungu.

   2. Waombee kwa imani na bidii katika mikutano yenu ya kila juma ya vikundi vya watatu, watu wa nchi hii ili wamkubali Yesu.
      a. Kila juma sali kuhusu habari unazozisikia radioni na runinga (televisheni) na kusoma katika magazeti ya Kikristo ambazo zingesaidia katika kuendeleza injili huko.
      b. Pata msaada wa sala kutoka kanisa au misheni yenye mawasiliano na kundi lako maalum la watu ambao hawajafikiwa na neno la Mungu.

   3. *Mwombee yule mwenye shamba awatume wavunaji wengi shambani mwake."* (Luka 10:2) Hii ni mahsusi kwa nchi yako katika dirisha la 10-40.

   4. Sali na kanisa lako, dini au mashirika mengine ambayo yamejitolea kuwaombea na kuwaongoa wopotevu ambao kamwe hawajasikia kuhusu Yesu.

SALA YAKO

1. Mwombe Bwana auweke mzigo wake wa waliopotea moyoni mwako.
2. Mwombe Mungu akuonyeshe taifa au kundi la watu ambalo anataka uwaombee.
3. Mwahidi Mungu kwamba utatii amri zake kuwaombea wapotevu ili wamkubali Yesu.
4. Mwombe Mungu akuelekeze kwa wanachama wengine wawili wa kikundi chako cha maombi ya watu watatu.

MAZOEZI

1. Watafute na kuwaandikisha wanachama wengine wawili wa kikundi chako cha watu watatu.
2. Tafuta nchi au kundi la watu lisilomjua Yesu.
3. Kitayarishe kikundi chako cha watu watatu kulingana na mapendekezo yafuatayo.
4. Omba kwa imani.

MASWALI NA MAJIBU KUHUSU KIKUNDI CHA SALA CHA WATU WATATU

JE, KIKUNDI CHA SALA CHA WATU WATATU NI NINI?

Kikundi cha watu watatu waliojitolea pamoja na mara kwa mara kuwaombea wapotevu.

TUWAOMBEE NANI?

1. Kila mtu katika kikundi huchagua watu watatu wasiomjua Yesu kuwa mwokozi na Bwana, na kufanya jumla ya watu 9 ambao mtawaombea.
2. Chagua taifa au kundi la watu ambalo halijafikiwa na injili ya Yesu. (Pata habari kutoka madhehebu au shirika lako, au shirika jingine linalo ombea ulimwengu, au tumia taifa ambalo mungu mwenyewe amekuchagulia)

NIWACHAGUEJE WASHIRIKA WANGU WAWILI KATIKA KIKUNDI CHA WATU WATATU?

Mwombe Mungu katika sala, akuonyeshe rafiki wawili wakristo, jamaa, au washiriki wa kanisa ambao anawataka wawe katika kikundi chako. Yapasa wawe wanaishi, kufanya kazi, au kuabudu karibu nawe kuwawezesha kukutana na kusali pamoja kila juma, watafute wengine walio na jukumu la kuwaombea wapotevu.

TUOMBE MARA NGAPI?

Mara moja kwa juma.

TUOMBEE KWA MUDA GANI KATIKA MIKUTANO YETU YA KILA JUMA?

Kwa muda usiopungua dakika 15 - au kwa muda ambao Mungu awataka muombe.

TUOMBE NINI?

1. Sala yenu ihusu tu uokovu wa watu wenu 9, na taifa lako au kundi lako ambalo halijafikiwa na neno la Mungu. (maombi mengine ya kuombewa yafanywe katika mikutano mingine ya sala, na si hapa.)
2. Ombeaneni wakati kila mmoja wenu anapojaribu kushirikiana na watu wake watatu na kuwaonyesha mapenzi ya Yesu, kwa vitendo.

TUSIFANYE NINI KATIKA MKUTANO WA SALA WA KIKUNDI CHA WATATU?

Msipoteze wakati mkiongea, ama mkila au mkinywa. Huu sio mkutano wa starehe ambapo maombi hufanywa mwisho, lakini wakati maalum wa kuwaombea wale wanaomhitaji Yesu.

TUOMBEE WAPI?

Mahali popote - kama kanisani, nyumbani, kazini na kadhalika.

TUENDELEE NA KIKUNDI HIKI KWA MUDA GANI?

Muamue kwanza mtaendelea kwa miezi mingapi, mwaka, na kadhalika. Mtaahidi kuomba pamoja. Fanyeni upya mkataba wenu baada ya muda huo.

MUNGU ATATARAJIA NINI KUTOKANA NA MAISHA YANGU

1. Kumbuka kwamba neno la Mungu lasema kwamba mtindo wa maisha yako unaofuata mapenzi yake Mungu, utaamua iwapo Mungu atayajibu maombi yako. Katika 1 Yohana 3:22, twaambiwa kwamba cho chote tunachomwomba, tutapokea, maana tunazitii amri zake na kufanya yale yanayompendeza.

MMOJA WA WALE TUNAOWAOMBEA AKIMKUBALI YESU, TUFANYE NINI?

1. Ikiwezekana, mshirikishe kanisani mwako, katika mafunzo ya Biblia, au ushirika, ukihakikisha ni mfuasi halisi wa Yesu katika maisha yake.
2. Usikome kumwombea.
3. Mtie moyo na msaidie mkristo huyo mpya ajiunge na kikundi cha maombi cha watu watatu ili naye ashiriki katika kuwaombea wale ambao bado hawajamjua Kristo.
4. Ongeza jina la mtu mwingine ambaye bado hajamjua Kristo ili muwe watu 9 tena na kuendelea na sala za kikundi cha watatu.

TUSHIRIKIANEJE NA VIKUNDI VINGINE VYA MAOMBI YA WATATU?

Ikiwezekana tayarisheni ratiba ya kikundi chako katika kanisa, dhehebu, shirika au jamii yako. Teua mwenyekiti wa kujua ni nani anayesali katika kikundi.

Toa taarifa za uamuzi wote uliochukuliwa kwa niaba ya Yesu, kwa mwenyekiti.

Kutaneni mara moja kwa mwezi ikiwezekana, kumsifu Mungu na kuombea ratiba ya kikundi chenu na pia kuombeana ninyi wenyewe.

KUOMBEA DIRISHA LA 10/40



DIRISHA LA 10/40

Himizo la juhudi za kueneza injili ulimwenguni katika miaka ya tisini inaelekea dirisha la 10/40. Eneo hili lililoko kati ya digrii 10 na 40 latitudi za kaskazini na laenea kutoka Uhispania na Afrika kaskazini hadi Japan na Ufilipino, lakisiwa kuwa 90% ya watu ambao hawajafikiwa na neno la Mungu ulimwenguni.

Hali juhudi za maombi lazima ziendelee katika miji na mataifa yetu, wito umetolewa ulimwenguni kupitia ushirika wa umoja wa maombi wa mwaka 2000 baada ya kristo, na baadaye, ukiwahimiza waombaji popote walipo washirikishe dirisha hilo la 10/40 katika maombi yao. Hapo ndipo twawapa makao makuu ya kimataifa ya dini za kiislamu, kihindi, kibudha, ki-confician, kishinto, kitao na kikomunisti. Maombi yenye nguvu ndiyo silaha kuu ya kuvunja ngome hizi za adui na kufungua njia kwa injili.

Ufanisi mkubwa umepatikana katika kueneza injili ulimwenguni katika karne yetu. Karibu watu wote wanaoishi nje ya dirisha la 10/40 wana nafasi nzuri ya kuisikia injili. George Otis Jr. alieleza vizuri zaidi katika kitabu chake mashuhuri kiitwacho (Jitu la mwisho).

> "Kwa ufupi, majeshi ya Bwana ya wenyeji sasa yamezizingira ngome za mwisho za nyoka - mataifa, na tawala za kidini katika dirisha la 10/40. Hali yakubalika kwamba jukumu lililobaki ndilo gumu zaidi katika vita vyetu, majeshi ya shetani yanakabiliwa na jamii ya waumini ambao nguvu zao za kiroho ambazo ikiwa zitatiwa hima, kuwasilishwa na kuunganishwa vizuri, kweli ni za kushangaza. (*Ukurasa 144*)
>
> Huu ndio mwito, nakupitia sala tutautekeleza
>
> C. Peter Wagne*
> Ushirika wa maombi wa mwaka 2000

*Ruhusa kuitumia imetolewa.